BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 28 Novemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. KIAPO CHA UAMINIFU CHA MHESHIMIWA MJUMBE WA BARAZA:

Mhe. Ramadhan Hamza Chande

II. TAARIFA YA SPIKA:

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 5 Oktoba, 2018.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Yanayosimamia Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria, Kurahisisha Upatikanaji wa Haki na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Yanayosimamia Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria, Kurahisisha Upatikanaji wa Haki na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

55. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Katika eneo la Michakaini “wireless” kuna mlima mkubwa ambao unaporomoka kila wakati kwa mvua kubwa na kuleta madhara baadhi ya wakati. Aidha, kuna sehemu ndogo katika mlima huo imejengwa kwa mtindo wa mawe na kuzuia mlima huo na pia kuleta haiba ya kupendeza katika mji.

(a) Je, Ofisi imeliona eneo hilo lilivyotengenezwa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza eneo hilo pamoja na milima mengine ili kuleta haiba nzuri katika mji.

(c) Je, ni nani aliyetengeneza eneo lile na kwanini hakumalizia mlima ule.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

61. MHESHIMIWA MOH’D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Naipongeza Serikali kwa kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma kwani wafanyakazi wengi wameweza kujiendeleza kimasomo wakiwa kazini, ili kujiongezea uweledi wa kutekeleza majukumu na kukuza mishahara yao. Lakini hivi karibuni kumejitokeza changamoto ya kutopandishwa mishahara ya wafanyakazi wanaomaliza masomo ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu tofauti na wafanyakazi waliomaliza masomo kipindi cha nyuma.

(a) Je, kwa nini wafanyakazi wanaomaliza Shahada ya Uzamili na Uzamivu wanapokea mishahara tofauti na wafanyakazi wenzao waliomaliza masomo yao kipindi cha nyuma wakati viwango vyao vya elimu vinalingana.

(b) Kuwepo kwa tofauti hiyo, je Serikali haioni inarudisha nyuma ari ya wafanyakazi kujiendeleza kielimu ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao.

(c) Je, ni lini Serikali itaweka sawa tofauti hiyo kubwa iliyopo na inayosababisha kuvunjika moyo kwa wafanyakazi kujiendeleza kielimu.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

77. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi kwa jitihada zake za kuwaanda na kuwapatia mradi vijana kwa lengo la kujikwamua kimaisha. Na kwa kuwa vijana wamekubali kujiajiri wenyewe ni jambo la kuigwa na wale waliokuwa hawajaandaa mabaraza kwenye shehia zilizo kuwa hazijaunda. Na kwa vile wananchi wamekuwa na uelewa juu ya afya zao.

(a) Je, ni nani hasa anayesimamia mradi huu baina ya Wilaya na Manispaa.

(b) Kwa kuwa wananchi wanatoa ushirikiano juu ya ukusanyaji wa fedha hizo ni kiasi gani wanachopewa vijana hao kwa kila mtu kuhusiana na mapato wanayokusanywa kwa mwezi.

(c) Na kwa kuwa wanafanyakazi hukusanya fedha nyingi kuna sababu zipi hadi kufikia miezi miwili bila kupewa malipo yao.

121. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kikosi cha KVZ kilichopo Kitogani kimemfukuza Asya Ali Mbarak ambae amekaa kambini kwa muda mrefu kwa kisingizio cha kushika ujauzito.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea kuondoshwa kambini.

(b) Je, sheria inasemaje kuhusu kushika ujauzito kwa mwanamke akiwa askari.

(c) Na je, wakati askari ameruhusiwa kuingia kambini “depu” madaktari waliohusika kumpima hawakumuona kuwa mjamzito, ambapo wamemuacha mpaka miezi mitatu na kumwambia ana ujauzito wa miezi mitatu na nusu.

<u>Wizara ya Fedha na Mipango</u>:

58. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Hivi karibuni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma alitoa taarifa katika vyombo vya habari akitaka wananchi watoe taarifa kwa Mamlaka husika kuhusu watendaji ambao wanamiliki mali nyingi tofauti na vipato halisi vya kazi zao.

(a) Je, Serikali imefanya utafiti kujua sababu gani watendaji wa sekta ya ununuzi na ugavi wanadaiwa kujihusisha na vitendo hivyo.

(b) Mbali na wito kwa wananchi, Je, ni mikakati ipi inafanyika kuhakikisha taasisi zote zinazojihusisha na ununuzi na ugavi zinafanyiwa uchunguzi na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi wakati wanapofanya michakato hiyo.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

3. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Makangale yenye wanafunzi 921 na walimu 19, ina changamoto kadhaa ikiwemo ya uhaba wa vyoo ambapo walimu na wanafunzi hao hutumia vyoo 6 tu. Aidha, pamoja na kuwepo kwa vifaa vya maabara, skuli haina chumba cha maabara. Pia skuli inakabiliwa na ufinyu wa ofisi za walimu, hivyo kupelekea walimu kukaa chini ya miti.

(a) Je, Wizara inazifahamu changamoto zote hizo, na kama inazifahamu ni hatua gani zimechukuliwa kukabiliana nazo ili kuleta ufanisi katika skuli hiyo.

(b) Je, Wizara kuigawa skuli hiyo kuwa ya msingi na sekondari haioni itaongeza gharama ambazo zingeweza kuepukika.

4. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa wanafunzi wa elimu mjumuisho wana changamoto kadhaa kama vile za huduma ya afya inapowabidi kwenda hospitali ambapo huchukuliwa kama wagonjwa wa kawaida na kupangwa foleni na baadhi ya siku hukosa huduma na kutakiwa kurejea siku nyengine. Hivyo, kuwakatisha tamaa hata kuacha kurejea tena au kupoteza muda wao wa masomo.

(a) Je, Wizara kupitia vituo vya afya kuna mpango wa kuwasaidia wanafunzi kwa kuwapangia utaratibu maalum wanafunzi wenye mahitaji maalum.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasiliana na Wizara ya Afya ili iweze kupitia skulini kuonana na wanafunzi wa elimu mjumuisho na kuwapatia huduma za afya na kutoa ushauri nasaha kulingana na mahitaji yao.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

22. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake za kuwaletea wananchi maendeleo kupitia sekta ya maji. Hata hivyo kuna kijiji cha Kiziwani Shungi, ambacho mpaka sasa hakijapata huduma ya maji safi na salama pamoja na Idara ya Maji kuahidi mara kwa mara kulitatua tatizo hilo.

(a) Je, ni tatizo gani lililosababisha kijiji hicho kutopatiwa maji safi na salama.

(b) Je, ni lini tatizo hilo litaondoka katika kijiji hicho.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo.

71. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji, na Nishati :

Upungufu wa mafuta wa kuendeshea vyombo vya usafiri Zanzibar limekuwa ni tatizo na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi.

(a) Je, ni tatizo gani linalosababisha upungufu wa mafuta.

(b) Je, kwa nini wakati wa kipindi cha utalii ndio hukosekana kwa huduma hiyo.

Wizara ya Afya:

1. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hospitali ya Wilaya ya Micheweni ina madereva wawili wanaoendesha gari za kubebea wagonjwa ambao hufanyakazi masaa 24 kwa kila siku za Jumamosi na Jumapili au skukuu. Hata hivyo, madereva hao hawalipwi “overtime” na “*call allowance*” jambo ambalo ni kinyume na

sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake na linapelekea kukosa hata muda wa mapumziko.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea kutolipwa "*over time*" kwa wafanyakazi hao.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwapangia zamu na kuwabadilisha madereva wa "Ambulace" ili na wao wapate muda wa kuendesha gari za vitengo vingine vilivyopo Wizarani.

(c) Je, Uongozi wa Wizara ya Afya Pemba ni lini utawalipa "overtime" madereva ambao wameshaendesha gari ya "Ambulace" kwa muda wa miaka miwili sasa bila ya kupatiwa malipo hayo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

46. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Sheria ya Usafiri Barabarani Namba 7 ya 2003 ambayo imetungiwa Kanuni zake ili iweze kutekelezeka vizuri na Kanuni hizo, zimetoa fursa na utaratibu mzuri wa huduma za usafiri kwa watu wenye ulemavu.

(a) Je, Wizara imechukua hatua gani ili kuhakikisha wamiliki wa vyombo vya usafiri wanafuata sheria hii ili watu wenye ulemavu kupata unafuu.

(b) Ni hatua gani hadi sasa zimeweza kuchukuliwa kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri vinavyowanyanyasa watu wenye ulemavu na ambavyo havifuati utaratibu wa Sheria na Kanuni kuhusiana na watu wenye ulemavu.

116. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Eneo la Mtoni tangu asili ni eneo la kuegesha meli aina ya "land craft". Lakini wadau wa meli hizo wanasumbuliwa na ZMA kuwa wasiegeshe meli hizo katika eneo la Mtoni na badala yake wameambiwa wakaegeshe eneo la Maruhubi.

(a) Je, ZMA imeangalia usalama wa eneo kwa vyombo hivyo.

(b) Je, ni sababu gani iliyopelekea kuwaondoa eneo la Mtoni ikiwa na hawa wawekezaji wazalendo wa nchi hii.

(c) Je, ZMA haioni kuwa inafanya makosa kwa vile hawana mamlaka ya eneo hilo, wenye mamlaka ni Shirika la Bandari.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Yanayosimamia Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria, Kurahisisha Upatikanaji wa Haki na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
28 Novemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.